



DECRA[®]
ROOFING SYSTEMS

**VIGAE HALISI VYA
BATI VYENYE NAKSHI
YA MIAMBA ASILIA**

NABAKI  **AFRIKA**
Quality Building Products

HERITAGE



HERITAGE

Kigae cha Decra® Heritage kina muonekano wenye mvuto na muundo uliokubalika na wasanifu wakuu tangu zamani. Wasanifu na wajenzi wa karne ya 21 wameendelea kuvutiwa na muundo huu wenye mtindo uliozoeleka na kukubalika. Decra® wameunda kigae hiki chenye historia maridadi kwa matumizi yanayokidhi mahitaji ya karne ya sasa.

MILANO



MILANO

Kigae cha Milano kimetengenezwa kulingana na ujenzi asilia wa Kirumi. Kigae hiki kina muundo mwanana wenye kuvutia – hasa kwenye paa lenye mwinuko mkali. Decra® Milano kimeundwa kutokana na mitindo iliyokubalika ya pembezoni mwa bahari Italia, na kinaipa nyumba yako muonekano upendezao kimtindo.



SHINGLE



SHINGLE

Decra® Shingle ni kigae cha muundo unaopendeza kwa usanifu wa kisasa au wa jadi. Kigae hiki kina muonekano wa paa la mawe na umbo lake thabiti linaipatia paa lako uimara na upekee. Kinapatikana kwa rangi tofauti asilia, na pia katika mpangilio wa kipekee wa rangi mbili kwa pamoja.



SHAKE



SHAKE

Kigae cha Decra® Shake kina muonekano ufananao na paa maridadi za mbao, na ziendanazo na paa za makuti. Kwa miaka mingi wajenzi na wasanifu wa pwani za Afrika waliezeka kwa makuti au mbao kwa nyumba zilizovutia kwa muonekano asilia. Kigae cha Decra® Shake kinaunganisha muonekano huo asilia na uimara wa teknolojia za kisasa za Decra® kwa kigae cha hali ya juu na cha kudumu.

FAIDA

USALAMA



Kigae cha Decra® kinaezekwa kwa kulazwa na kufungwiwa kwenye kigae cha juu yake, kigae cha chini yake, vigae viwili pembezoni mwake NA PIA kwenye rafta. Hii inafanya paa la Decra® kuwa paa thabiti na salama kinyume na wizi au upepo mkali.

KUPIMWA NA KUKAGULIWA



Kila kigae cha Decra kinakaguliwa kwa mkono kuhakikisha ubora unaofanana kwa vigae vyetu vyote. Pia sisi hupima bidhaa zetu na za washindani wetu kwenye maabara yetu kuhakikisha kuwa Decra® inazidi kuwa bora kuliko kigae kingine chochote.

UZITO



Kwa kuwa na kilo 7 tu kwa kila mita ya mraba (7.0kg/m^2), kigae cha Decra® kinaweza kukuokolea gharama kubwa za muundo wa paa lako (yaani rafta, kenchi, papi n.k.), msingi na usafiri. Tani 1 ya vigae vya Decra® inaezeka sawa sawa na tani 10 za vigae vya saruji au vya udongo.

UJENZI WA PWANI



Vigae vya Decra® vimethibitishwa kuwa na uwezo wa kudumu kati ya mara 6 mpaka 9 zaidi ya mabati ya kawaida. Kama unaishi pembezoni mwa bahari, Decra® ndiyo chaguo sahihi kwako hasa kwa sababu ya waranti yetu ya miaka 50 iliyoandikwa.



UTENDAJI KATIKA HALI YA HEWA

Vigae vyetu vinapimwa kwenye tufani yenye nguvu ya kilometa 200 kwa saa (200kph) katika Maabara ya Utafiti wa Ujenzi iliyoko Miami na Stesheni ya Kupima Vimbunga iliyoko Australia.



HISTORIA

Sisi ndiye tuliovumbua kigae cha chuma mwaka 1957. Hakuna kampuni iliyo na uzoefu tulionao katika kukuletea ubora na uimara.



KUPAMBANANA MOTO

Vigae vya Decra® hupimwa kwenye joto la mpaka nyuzijoto 760°C na katika vipimo hivyo havikuonesha moto, cheche au moshi. Hii ni mathubuti zaidi kwenye maeneo yenye joto kali na kwenye majengo ya kibiashara au ya umma.



MUDA MFUPI WA UEZEKAJI

Vigae vya Decra® vinaezekwa kwa haraka na kwa sababu hiyo vinaweza kukuokolea gharama nyingine zinazojitokeza kwa muda. Hii huamisha unaweza kuhamia nyumbani kwako mapema zaidi.

